**Muda>>**Maofisa washikilia ng'ombe tangu mwaka 2017

# Waziri Mpina atoa msimamo mifugo iliyokufa hifadhini

NA MWANDISHI WETU, SIMIYU

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, ametoa msimamo kuhusu ng'ombe zaidi ya 1,400 za wafugaji wa Wilaya za Itilima na Meatu mkoani Simiyu, zinazodaiwa kufa mikononi mwa Maofisa wa Pori la Akiba la Maswa, baada ya kushikiliwa hifadhini kwa kipindi cha miaka mitatu.

Kutokana na hali hiyo, amewaagiza Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu kuitisha kikao cha pamoja kitakachomhusisha Mhifadhi Mkuu wa Pori la Maswa, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo Tanzania na Mwanasheria wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi na wafugaji wanaolalamikia kudhulumiwa mifugo yao.

Agizo hilo limekuja mara baada ya kupokea malalamiko kutoka wafugaji kuwa ng'ombe zao zilishikiliwa bila kupatiwa huduma muhimu za chanjo, dawa, maji na malisho licha ya Mahakama kutoa hukumu kwa wamiliki kurejeshewa mifugo yao.

Pia, Waziri Mpina, aliagiza wafugaji wote mkoani Simiyu walioshinda kesi mahakamani na kutakiwa kurejeshewa mifugo yao, kuwasilisha vielelezo vya hukumu za kesi hizo kwenye ofisi za Wakuu wa Wilaya za Itilima na Meatu ili haki iweze kutendeka

Katika malalamiko yao, wafugaji hao, walisema tangu mwaka 2017, ng'ombe 1, 484 zilikamatwa kwa madai kuwa zilikuwa ndani ya pori hilo licha ya Mahakama kuamuru warudishiwe ng'ombe zao bado waliendelea kushikiliwa na kuendelea kufa na kubaki 72.

Wakitoa kilio chao mbele ya Waziri Mpina aliyefika katika vijiji vya Laini A na Laini B wilayani Itilima, Mwangudo na Malwilo wilayani Meatu mkoani Simiyu, wafugaji hao, walisema licha ya Mahakama kutoa uamuzi warejeshewe mifugo yao lakini bado hawajarudishiwa.

Baadhi ya wamiliki wa mifugo hiyo, walioshinda kesi kwa upande wa Itilima ni Malimi Sendama, Ngasa Mbeho, Kongwa Tulutu na Maduhu Mbuli, ambao walimkabidhi Waziri Mpina risiti mbalimbali zinazoonesha mifugo hiyo kuuzwa kwa bei ya hasara.

Wafugaji wengine kutoka Meatu waliodhulumiwa ng'ombe 345 ni Subi Maduhu, Masunga Muhamali, Zengo Kusekelwa, Kija Badila ambao mifugo yao inadaiwa kufa huku mfugaji mwingine akidai kuwa ng'ombe zake 55 ambapo Mahakama iliamuru alipe faini ya sh. milioni 1.4 ili arudishiwe na alilipa lakini mifugo yake haijarudishwa hadi sasa.

Akiwasilisha kilio kwa niaba ya wafugaji hao, Katibu wa Mbunge wa Itilima, Alex Ngulukulu, alisema wahifadhi hao walitoa maelezo kuwa ng'ombe 289 wamekufa jambo ambalo siyo la kweli kwani askari wa hifadhi walikuwa wanaendesha minada ya kuuza mifugo hiyo.

Diwani wa Kata ya Tindabuligi, Tabu Maghembe, alisema maelezo yaliyotolewa na askari wa hifadhi hiyo, kuwa mifugo imekufa hawakubaliani nayo kwa sababu hakuna mlipuko wowote wa magonjwa ulioripotiwa katika kipindi hicho.

Kutokana na hali hiyo, walimuomba Waziri Mpina kufikisha kilio hicho cha wafugaji wa Itilima na Meatu kwa Rais Dk. John Magufuli ili aingile kati, waweze kupata haki yao kwa sababu kwa muda mrefu amekuwa akipigania haki za wanyonge.

Mbali na malalamiko hayo, pia wafugaji hao walilalamikia kitendo Maofisa wa Pori la Akiba Maswa kutanua mpaka bila kuwashirikisha na hivyo kuendelea kupunguza eneo la malisho na kusababisha usumbufu mkubwa kwa wafugaji.

Pia, wananchi wa Wilaya za Wilaya za Maswa na Meatu, wamelalamikia mgogoro wa mpaka katika Ziwa Kitangiri kuwa wamekuwa wakizuiliwa kuvua na kukamatwa kwa sababu wameingia wilaya ya Iramba Mkoa wa Singida.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Juma Mpina, alimshukuru Rais Dk. John Magufuli kwa kuruhusu matumizi ya mita 500 kutoka kwenye Pori la Akiba la Maswa yatumike kwa shughuli za kulishia mifugo.

Pia, kuruhusu matumizi ya mita 60 kutoka kwenye mto kutumika kwa shughuli za kunyweshea maji mifugo yao jambo ambalo hapo kabla wananchi walikuwa wakizuiliwa na kusababisha mifugo mingi kufa kwa kukosa maji na malisho.

Kuhusu kuvua samaki Ziwa Kitangiri, Waziri Mpina, aliagiza Kamishna wa Ardhi, Mkurugenzi wa Uvuvi Tanzania, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Meatu na Mkurugenzi wa Iramba ili kupitia upya mipaka hiyo na kumaliza kabisa mgogoro huo kuhusu uvuvi katika Ziwa hilo.

Akizungumzia suala la kupanua mpaka kiholela, Waziri Mpina, aliagiza timu ya Wataalamu kutoka Wizara nane kupita kwenye maeneo yanayolalamikiwa na kupima upya mipaka hiyo kwa uwazi na kwamba wananchi watashiriki katika zoezi hilo.

WAZIRI MPINA




**WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina, akisalimiana na wananchi alipowasili Kijiji cha Mwangudo, Wilaya ya Meatu, mkoani Simiyu. (Na Mpigapicha Wetu).**

Scanned by CamScanner

Hospitali Chake Chake, ingawa kwa sasa ni mapema kutoa majibu ya vipimo hivyo, hadi hapo wakati utakapofika.

baada ya wiki moja kupita akiwa hajui nini kinachoendelea, alifikwa na sheha wake na

MAKATIBU WAKUU



MAKATIBU Wakuu wenye dhamana ya maafa kwenye Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kutoka Tanzania, wakihudhuria kikao chao kilichoanza juzi, mjini Unguja. Kutoka kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Dk. Faraij Mnyepe, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Olesante Ole Gabriel na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Christopher Kadio.

# Ripoti ya Kamati yabaini udhaifu katika utendaji

NA EMMANUEL MOHAMED, ZANZIBAR

maeneo mbalimbali yakiwemo ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato na taratibu za

zilizokosa vielelezo vya malipo husika uhesabiwa kuwa hati hizo hazipo na malipo hayo ni batili kwa kukosa uthibitisho halali

UHURU
MAONI YA MHARIRI

# Wafanyabiashara wa Bucha wanapaswa kutii maagizo ya Bodi ya Nyama nchini

JANA gazeti hili lilikuwa na habari kuhusiana na uamuzi wa Wizara ya Mifugo kupitia Bodi ya Nyama (TMB), kurudia kutoa onyo dhidi ya matumizi ya magogo kukatia nyama mabuchani na kusema kuanzia Jumatatu itapita bucha hadi bucha kufanya ukaguzi wa kina.

Uamuzi na onyo la Bodi ya Nyama unastahili pongezi hasa ikizingatiwa umelenga katika kuhakikisha kila kipande cha nyama kinachouzwa au kutolewa kwa ajili ya matumizi ya binadamu kinakidhi vigezo vya afya.

Pia, magogo yanayotumika kukatia nyama yana athari kiafya, hivyo ujeuri unaoendelea wa baadhi ya wafanyabiashara wa mabucha ya nyama kwenye maeneo mbalimbali nchini ni kuhatarisha usalama wa walaji wa nyama nchini.

Kimsingi jamii inapaswa kutambua kuwa mfanyabiashara yeyote anayetumia magogo buchani anafanya makosa na hatua za kisheria dhidi yake zinapaswa kuchukuliwa ili kumlinda mlaji.

Lazima tulinde afya za kila mtanzania hasa wanaotumia mabucha kupata vitoweo vyao, ambavyo kwa namna moja au nyingine vina matatizo kwa binadamu, hivyo umefika wakati wa kukomesha tatizo hilo.

Tunapongeza operesheni ya kusaka mabucha inayoendelea lakini iwe endelevu na wengine ambao hawajafikiwa na operesheni wanapaswa kuchukua hatua za kuachana na matumizi ya magogo.

Pia, watendaji wa wizara na wengine kutoka mamlaka zingine wawe mstari wa mbele kuhakikisha magogo yanaondolewa kwenye mabucha ili kulinda afya za walaji.

Kwa wafanyabiashara wanapaswa kubadilika na kutumia mashine za ukataji nyama ambazo ni salama na zenye ubora wa hali juu, badala ya kuendelea kuhatarisha afya za walaji kwa magogo hayo.

Tunaamini serikali licha ya kuendesha operesheni pia itatoa elimu kwa wafanyabiashara na umma kwa ujumla ili waondokane na matumizi ya magogo hayo kwa maslahi mapana ya taifa.

Japokuwa kuna malalamiko kwa wafanyabiashara ikiwemo kulalamika gharama za mashine za kukatia nyama, lakini hilo lisiwe kikwazo kwa serikali kuhakikisha inaondokana na matumizi magogo kwenye mabucha.

Kwa mantiki hiyo, huu ni wakati wa wafanyabiashara kutii maagizo ya serikali ya kuachana na matumizi ya magogo kwenye mabucha, ambayo yamekuwa na madhara makubwa kwa walaji na vile vile kuhatarisha soko la bidhaa hiyo.

Scanned by CamScanner

## HOJA YA HAJA

**Mkakati>>**Msako wa magogo kwenye mabucha kufanyika nchi

**Ndiyo maana ikafungua milango kwa wawekezaji ambao wana lengo la kuwekeza kujitokeza na kuwekeza katika ardhi ya Tanzania.**



Na ERICK MINYAVU

# Ufugaji samaki unavyochangia kuwaondoa vijana vijiweni

UFUGAJI wa samaki unazidi kukua nchini na kuwa chanzo cha ajira kwa wananchi hususan vijana kutokana na muitikio wake katika suala hilo.

**Tumeona namna ambavyo serikali inajitahidi kila kukicha kuboresha na kuweka mazingira mazuri ambayo yatarahisisha suala la ufugaji.**

Hatua hiyo inatokana na wananchi kuwa na mwamko wa kuanza kufanya shughuli hiyo, ambayo inachangia maendeleo na ukuji wa pato la taifa.

Pia imechangia kwa kiwango kikubwa vijana wengi kuacha kukaa vijiweni na kufanya mambo yasiyokuwa na maadili kwa jamii.

Tumeona namna ambavyo serikali inajitahidi kila kukicha kuboresha na kuweka mazingira mazuri ambayo yatarahisisha suala la ufugaji.

Kutokana na hilo, sekta ya ufugaji imekuwa kwa kiwango kikubwa ikilinganisha na hali ya zamani ambapo suala la ufugaji samaki lilikuwa si kwa ukubwa.

Hivi sasa wafugaji wanazalisha zaidi ya tani 400,000 huku hitaji likiwa ni tani 800,000 hii inaonyesha namna gani watu walivyohamasika.

Pia sekta ya uvuvi imekuwa na mchango mkubwa katika pato la taifa kwani mpaka sasa uvuvi inachangia kwa asilimia 1.7 huku ikitoa ajira kwa watu milioni 4.5.

Ikumbukwe awali samaki walikuwa wakiagizwa nje ya nchi lakini kwa sasa jambo hilo halipo tena kutokana na wananchi kufuga samaki wa aina tofauti.

Mbali na mafanikio hayo changamoto kubwa ambavyo imekuwa ikiendelea kuikumba sekta hiyo ni aina ya chakula bora.

Wafugaji wengi wamekuwa wakilalamikia upatikanaji wa chakula bora cha kwa ajili ya samaki kuwa mdogo ukilinganisha na ufugaji ambao unaendelea kukua kila siku nchini.

Hivyo hii ni fursa kwa wawekezaji kujitokeza na kuweka nguvu zao katika hili ili kuhakikisha sekta hiyo ya uvuvi inazidi kupanuka.

Kutokana na hilo serikali imekuwa ikiunga mkono sekta binafsi ambazo zimekuwa kichocheo cha maendeleo ya nchini.

Ndiyo maana ikafungua milango kwa wawekezaji ambao wana lengo la kuwekeza kujitokeza na kuwekeza katika ardhi ya Tanzania.

Pia kwa kuzidi kulifanyia kazi hilo Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, aliwaahidi wafugaji wa samaki katika bajeti ya mwaka huu atajitahidi kupendekeza kuwekwa kwa msamaha wa kodi kwa vifaa vya ufugaji wa samaki.

## TULIKOTOKA

Scanned by CamScanner